MRADI WA KIMATAIFA WA KIFEMINIA
MAFUNZO LINGANISHI YA NCHI MBALIMBALI YA
HARAKATI YA WANAWAKE NA JINSIA
NA USOMI

NCHI: TANZANIA

Jina la Mhojiwa: Sabrina Othman Faraji

Jina la mhojaji: Anneth Meena

Mahali: Unguja, Zanzibar

Tarehe: 12/15/2022

Chuo Kikuu cha Michigan
Taasisi ya Utafiti wa Wanawake na Jinsia
1136 Lane Hall Ann Arbor, MI 48109-1290
Simu: (734) 764-9537

Barua Pepe: um.gfp@umich.edu
Tovuti: http://www.umich.edu/~glblfem

© Regents of the University of Michigan, 2022

Sabrina Othman Faraji ni mjasiriamali, mwanamitindo, na mwanaharakati ambaye amebobea kwenye kujengea uwezo wa wanawake kiuchumi hususani wanawake wapembezoni pamoja na vijijini. Bi. Sabrina anafundisa wanawake kozi za ushonaji na stadi za ujasiriamali hasa kwa wanawake wanaoishi na virusi vya Ukimwi. Vile vile, hutoa ajira kwa wanawake alioawapatia mafunzo ya ushonaji kwenye kampuni yake ijulikanayo kam Khanga Kabisa; Bi. Sabrinai amebobea kwenye tasnia ya mitindo tangu mwaka 2007 mpaka 2013 na baadaye kukuwa na kufikia kuwa meneja uzalisha kwenye kampuni kuanzia mwaka 2013 mpaka sasa hivi.

Bi. Sabrina ni miongoni wa waraatibu wa Tamasha la Kimataifa la FIlamu Zanzibar, anaratibu program mbalimbali ikia ni pamoja na shughulizi za kijamii kama vile mbio za marathoni, usafi wa ufukwe, warsha za uwezweshaji kiuchumi kwa wanawake, maonesho ya kazi za mikono kwa ajili ya Tamasha la Filamu la Kila Mwaka, nafasi hii ameshika tangu mwaka 2000 hadi hivi sasa.

Bi. Sabrinai ametunukia tuzo mbalibali ikiwa ni pamoja na mfanya biashara wa mwaka mwanamke inayotolewa na wizara ya Biashara Zanzibara; Tuzo ya mradi bora iliyotolewa na Jukwaa la Wanawake la Biashara; na Tuzo ya Huduma bora kwa Jamii inayotolewa na Tamasha la Kimataifa la Filamu la Zanzibar.

Bi. Sabrina anajihusisha na miradi mingine kama vile utengenezaji wa taulo za kike zijulikanavyo kama *Lily Pads*.

Bi. Sabrina ana Stashahada ya Usimamizi wa Biashara na Utawala wa Umma kutoka Chuo Kikuu cha Zanzibar, Tanzania.

Anneth E. Meena, alizaliwa 1971, ni mtafiti, mwanaharakati na mfeminia. Bi. Meena ni mshauri wa kujitegemea kwenye maeneo mbalilmbali ikiwa ni pamoja na mazingira, Afya na maswala ya Jinsia. Amefanya kazi na mashirika mbalimbali kwenye nafasi mbalilmbli ikiwa ni pamoja na mratibu wa ufuatiliaji na tathmini World Vision, ofisi ya Arusha (2000); Mratibu wa mradi wa Kituo vya Ubora na Ufanisi kupitia shirika lisilo la kiserikali lijulikanalo kama Jukwaa la Wanaelimu Wanawake wa Kiafrika ambapo program hii ilibobea katika kuzingatia jinsia katika mtaala na ufundishaji unaozingatia jinsia (2001 - 2002). Alikuwa mmoja wa waasisi wa shule ya sekondari ya upili iliyojulikana kama Raida akiwa meneja wa kwanza wa shule na baadaye kuwa mkuu wa chuo cha kati wa kwanza (2007 - 2017). Bi. Meena amefanya kazi kama mshauri wa kujitegema katika mashirika mbalimbali ya haki za wanawake yakiwemo TGNP Mtandao; Mfuko wa Wanawake Tanzania; Soma. Vile vile amefanya kazi za tafiti mbalimbli ikiw ni pmaoja na mabadiliko ya tabia nchi na Taasisi za elimu ya Juu ikiwa ni pamoja na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania na Chuo Kikuu cha Michigan, Marekani.

Ms. Meena ni mwanachama wa mitandao mbalimbali kama vile mtandao wa kupinga rushwa ya ngono, mtandoa wa haki ya uzazi, ujinsi na afya.

Bi. Meena ametunukiwa tuzo mbalimbali za kitaaluma ikiwa ni pamoja na Tuzo ya Hammad kwa kutambua kazi ya kipekee yenye mada ya kimataifa iliyotolewa na shule ya Huduma za

Umma ya Wagner, Chuo kikuu cha New York Marekani. Vile vile ni miongoni mwa wanawake wawili wa Africa waliopata udhamini wa masomo kutoka kwa Oprah Winfrey na kusoma katika Chuo Kikuu cha New York, Marekani katika kipindi cha 2004 - 2005. Pia amepokea udhamini wa Ford Foundation na kupata nafasi ya utafiti katika kituo cha Kimataifa cha Utafiti wa Wanawake, Washington, DC, Marekani mwaka 1999. Amepokea tuzo ndogo ya utafiti kutoka Baraza la Maendeleo ya Utafiti wa Sayansi ya Jamii.

Ms. Meena ana shahada ya kwanza katika sayansi ya Mazingira na Jiografia kutoka Chuo Kikuu cha Cape Town, Cape Town, Afrika ya Kusini (1996). Shahada ya Uzamili ya sayansi ya watu (Demografia) kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania (2000); na Shahada ya Sayansi katika Usimamizi wa Huduma za Umma kutoka chuo Kikuu cha New York, New York, Marekani (2005).

Anneth Meena: Hello, habari za asubuhi dada?

Sabrina Othman Faraji: Nzuri hujambo?

AM: Sijambo asante kwa muda wako.

SOF: Karibu!

AM: Asante naomba tuanze, kama uko tayari.

SOF: Inshallah! Tuanze

AM: Ok! Karibu kwenye utafiti wetu wa wanawake na jinsia mradi wa kimataifa wa kifemenia udahili huu ni sehemu wa mradi wa kimataifa wa kifemenia ambao ni mradi wa kimataifa unaothaminiwa na chuo kikuu cha Michigan. Lengo ni kukusanya taarifa za kihistoria na kuzihifadhi hasa mazungumzo ya wanawake ambapo uanaharakati wao huchangia kwenye mapambano ya kiharakati na mambo muhimu ya wanawake. Hivyo basi tutatumia takribani lisaa limoja kujadili maeneo makuu Matano: Maisha yako kwa ujumla, tafakari yako ya kazi, maoni yako kuhusu mahusiano kati ya ufemenia na harakati na hivyo kuhusiana na kazi zako, mtazamo wako na maoni yako kwenye mtazamo mzima wa takwa la wanawake ama women movement, mahusiano yaliyopo kama yapo kati ya kazi unazozifanya na hizo za wanaharakati wengine nchini.

Hivyo basi kwa kuanzia tunaanza na historia ya maisha yako. Unapofikiria kuhusu ulipo leo unaonaje safari yako ilipokufikisha leo kwa sasa kazi yako unaweza kusema nini katika kazi yako na ni nini unaweza kusema unajivunia kama mafanikio yako makubwa katika kazi yako. Kwa hiyo mtazamo wako kwa kazi yako mpaka hapo ulipofikia ni kitu gani unaweza kujivunia kuhusu kazi yako. Karibu!

SOF: Jina langu naitwa Sabrina Othman Faraji.

AM: Asante

SOF: Ni mama wa watoto watatu nimesoma primary na secondary nilifikia hapo kwa sababu mamangu hakuwa na uwezo wa kuweza kunisomesha alinilea yeye peke yake bila ya baba. Na yeye ndiye aliyenifanya nikawa jasiri, na nikahamasika kutokuweza kuendelea kusoma nikaanza uanaharakati. Nilianza kupambana na uharakati nilipokuwa mdogo sana baada ya kumaliza shule tu. Nikaingia katika mapambano ya kuanza kutafuta maisha, nilikutana na wanaume, nilianza kufanya kazi katika NGO moja ambayo ilikuwa na wanaume watupu mimi peke yangu nilikuwa mwanamke na nilikuwa ni kiongozi. Kwa sababu nilikuwa na elimu ndogo lakini elimu yangu ya sekondari kwa kipindi hicho elimu yangu ilikuwa kubwa kwa sababu nilimaliza A level. Ambao nilikutana nao walikuwa wote hawana elimu na mimi nilikuwa nazungumza lugha tofauti na wao. Kwa hiyo nilikuwa kiongozi katika organization ya women center ambayo tulikuwa tunasaidia wanawake kuweza kuwasaidia kusoma lugha kwa ajili ya kutembeza wageni. Tukafanya mchakato huo

kwa muda mchache baadae mimi nikajiunga na Zanzibar international feeling festival ni tamasha la nchi la majahazi nikaingia hapo nikawa kama mwanamke ambae nashughulikia harakati za wanawake kuwahamazisha wanawake pamoja na watoto na pia kutayarisha majukwaa maalum. Nilikuwa naenda vijijini kuwahamazisha wanawake jinsi gani wanawake tunaweza kupambana na kufanikiwa. Katika kipindi chote hicho sikuwa hapo tu nilifanya kazi pia katika hotel nilikuwa ni msaidizi meneja. Na pia nikakutana na hawa wa Swedish ambao wenye hii kampuni ambayo naendesha sasa hivi wao ndio walioniambia niache kazi katika NGO ya kusaidia wanawake na niweze kuanza biashara. Sikusomea mambo ya text time lakini wao ndio walioniona ujasiri wangu na ukakamavu wangu ndipo nikaingia katika mchanganuo huo wa kuanza kuingia kwenye biashara. Nilisimamia kazi kwa kipindi fulani nilikuwa nasimamia dukani pamoja na kukusanya mapato yote ya fedha pia mimi ndio niliyekuwa msimamisi wa kwenda kununua vitambaa Dar es Salaam na kurudi na kipindi hicho chote nilikuwa bado ni mdogo na sijaolewa. Na nilikuwa na kiu sana ya maisha kwa sababu mamangu alikuwa ni masikini alishindwa kunisomesha. Kwa hiyo nikaweza kujitambua kama mimi mwanamke na pia nategemewa kuwa ni mama na kuweza kuendesha jamii kama mamangu alivyoweza kunisomesha kuwa na mimi nina jukumu la kuja kuwalea watoto wangu. Kwa hiyo nikapambana kadri niwezavyo nilikuwa nafanya kazi kwa jitihada kubwa kwa sababu unajua wenzetu wa nje ni tofauti na sisi na tamaduni zetu na pia mimi ni muislam. Ilikuwa vigumu sana kwa sababu mimi nilikuwa natakiwa niende hotel kufuatilia order lakini nilijitoa kama mwanamke kuweza kupambana na kukutana na watu tofauti wa kunipa mawazo, wao ndio walioweza kunifanya niweze… [muted]

AM: Hello naona umekwama kidogo

SOF: Okay. Unanisikia sasa?

AM: Ndio nakusikia

SOF: Sawa. Na kipindi chote hichi mimi nilianza kuwasajilisha kuweza kuwachukua wanawake wenzangu ambao wamemaliza shule wanakaa nyumbani bila kazi. Kwa hiyo nikaanza kuwafundisha hapa kanga kabsa na kuwafundisha kwa sababu mwanzo kabsa tulikuwa tunashona sare tu ila sasa hivi tunafanya vikoi pamoja na sanitary pad, kwa hiyo nikaanza kuwafundisha jinsi ya kutengeneza vikoi kutengeneza pedi za wanawake na pia mpaka sasa nina wanafunzi ninaowasomesha ili na wao waweze kujisimamia kama wanawake wapambane kama nilivyopambana mimi kwa sababu mimi sio mfanyakazi tena mimi sasa ni boss wa kuendesha ofisi hii na kuwaajiri watu.

AM: Hongera sana na asante sana. Historia ya maisha yako ya kazi umeongelea kidogo lakini pia ungeweza kugusia vitu ambavyo hukuvisema kwa mfano; nini kilikuhamazisha katika kazi unayoifanya je ulifikiaje kufanya kazi unayofanya umeongelea kidogo na je kama kumekuwa na mabadiliko gani, kazi yako imebadilishwa na uzoefu wa maisha yako? Je umekuwa na mabadiliko binafsi kutokana na kujihuzisha katika harakati na ni sehemu gani ambayo wewe umebobea ya uharakati. Karibu

SOF: Asante. Mimi katika kitu ambacho kilinihamazisha kuingia katika kazi kwa sababu mimi mwenyewe sikuwa najielewa kama naweza kuendesha biashara au na mimi nina kitu ambacho kimo katika damu yangu kama mambo ya vitambaa na fashion. Sasa hao walioniongoza ndio walioweza kunijua kuwa mimi nina kitu ambacho ni zawadi na ninaweza nikawapa wenzangu. Kwa hiyo hicho ndicho ambacho kilinivutia katika kazi yangu nilipojitambua kuwa kumbe mimi nina maarifa haya kwa hiyo na mimi ndipo nikaingia huko.

AM: Okay, endelea samahani.

SOF: Na kazi yangui imeleta mabadiliko kwa sababu mimi mabadiliko niliyopata mimi nilikuwa ni mfanyakazi tu lakini sasa hivi mimi ndio nimekuwa naongoza ofsi, naajiri watu, nakutana na watu tofauti. Na mimi pia naweza kusimama pahali popote kusema kuwa na mimi pia namiliki kitu fulani, kwa hiyo hayo ndio mabadiliko niliyoyapata katika hii kazi. Kwa sababu kwanza sikuanzia kazi hii mwanzo mimi nilikuwepo katika NGO kusaidia wanawake na mambo mengine. Kwa hiyo mabadiliko niliyoyapata ni kuweza kuwa nimetoka katika kuwa mfanyakazi sasa hivi mimi ndio nawaajiri watu.

AM: Okay. Na hiyo kazi yako ninagusaje maisha ya wanawake labda kwenye harakati na watoto.

SOF: Okay! Kazi yangu hii inawagusa wanawake kwa sababu nawasajilisha wanawake wenzangu, kuwasomesha na kuweza kujifunza kushona na wao waende katika sehemu zao wakawafundishe na wanawake wengine kwa sababu wanawake wengi wanateseka hawana kazi. Kwahiyo wakishasoma hapa wakaenda zao majumbani wakaenda zao majumbani na kuwafundisha na watu wengine kwa hiyo na wanawake wengine watapata kujikomboa na wao wataweza kuwa na kazi ambazo wanaweza kujitegemea wenyewe bila kumtegemea mtu mwingine na kuwasaidia watoto wao. Na mbali na hilo kunakuwa na raw materials ambazo hizi raw materials inawasaidia watu ambao wameathirika na ukimwi nawapa vile vitambaa wanaweza kutengeneza vitu kama domements or small porches. Kwa hiyo pia ni contribution yangu katika jamii kuwakomboa wanawake wengine kuweza kujisaidia katika maisha.

AM: Asante. Tukija sehemu ya tatu tunaongelea tafakari ya maisha yako. Kwenye hapa tunakuuliza kwa mfano; unaelewaje neno feminia/uanaharakati maana yake ni nini kwako?

SOF: Okay! Kwangu mimi uanaharakati ni wewe mwenyewe kuweza kujitambua na kujithamini kuwa mwanamke na kujitoa kuweza kutimiza wajibu wako na malengo yako ya maisha ambayo umejipangia.

AM: Okay. Je inamaana gani katika kazi yako?

SOF: Katika kazi yangu uanaharakati unamaana kuwa kukutana na watu kubadilishana mawazo kupata mambo mbalimbali kwa mfano ukikutana na watu wanajua unafanya kazi

gani, unapata orders, unapata kujulikana, unapata mchanganuo wa maisha kumbe hapa nilipo kuwepo sitakiwi kuwepo hapa tu natakiwa niende mbele zaidi.

AM: Sawa. Na vile vile kwenye kazi yako pia umesema unasomesha wanafunzi kwa hiyo pia unagusa maisha ya watu mbalimbali si ndiyo?

SOF: Ndio nasomesha wanafunzi ndio nasomesha wanafunzi kujua kutengeneza vikoi, kutengeneza sanitary pad.

AM: Na wao wanapata ujuzi wanapeleka sehemu zao wanazotokea.

SOF: Na wengine pia nawaajiri hapa hapa.

AM: Aah! Baada ya kufundishwa kuna ambao unawaajiri.

SOF: Ndio ambao watakuwa wanalingana na sifa zangu za kazi wanabakia hapa hapa.

AM: Kwa hiyo pia unayo ile kuwahakikisha kuna ambao wanapata ajira na kuna ambao wanaenda kujiajiri.

SOF: Ndio wengine wanaenda kujiajiri wenyewe.

AM: Okay. Na ni watu mbalimbali pamoja na watu walioathirika umesema wanawake walioathirika.

SOF: Ndio na wanawake walioathirika na wanawake wengi ambao wanakuja hapa ni wale wanawake wanaotoka vijiji tofauti kama Makokotoni wanatoka Nungwi wanatoka Makunduchi, Bumbwini kama kwa mfano nikienda kwenye harakati zangu nikikuta watu wanashida kwa hiyo yule namchukua namleta kuweza kumsaidia ili na yeye ajinyanyue kwa hiyo mwenyewe nikiona huyu anafaa kuwepo hapa atabakia nikiona au namuuliza mwenyewe anaweza kujiendeleza mwenyewe nyumbani na maisha yake.

AM: Okay, kwa hiyo wewe unaenda kuwatafuta huko vijijini?

SOF: Ndio, kwa sababu kama nilivyokwambia mimi nafanya kazi pia katika tamasha la nchi la majahaz na mimi ni coordinator wa jukwaa la wanawake. Kwa hiyo nakuwa natembelea vijiji kwaajili ya kuwahamazisha wanawake kwenye film, kuhamazisha wanawake kuweza kujitegemea, nahamazisha wanawake kwa kupitia nyanja mbalimbali. Kwa hiyo nakutana na watu wengi huko nikienda na najua jinsi gani wanavyohangaika wanawake na maisha.

AM: Okay! Asante. Kwenye sehemu yetu ya nne tunaongelea mahusiano ya feminia na harakati. Je nini mtazamo wako kati ya ufemenia na uharakti unaelewaje hiyo kwa ujumla katika kazi yako.

SOF: Okay! Feminia na uanaharakati kwangu mimi ninavyoufahamu kwa ufahamu wangu mdogo kwa sababu ufeminia ni mambo yanayohusu wanawake na harakati ni mambo yako

mwenyewe kama wewe binadamu unavyojipangia. Mimi nafanya kazi na hotels kwa hiyo natakiwa nifanye hivi, nikutane na hawa na ufeminia ni uwanawake ni ujike. Sasa mimi ninavyofahamu uanaharakati na ufeminia ni mwanamke na utaratibu mzima wa shughuli zake ambazo anazifanya na kujipangia kwa kila siku. Sijui labda wewe unavyofahamu wewe zaidi ya mimi.

AM: Ufemenia inahusu wote wanawake na wanaume ni ile kuzikataa zile mila potofu mifumo kandamizi na uanaharakati ni hivyo vitu unavyofanya kwenye kumkomboa mwanamke na mtoto katika ukandamizwaji. Kwa hivyo we unasema unazifanya hizi kazi za kila siku ni kwenye kujikomboa wewe binafsi na hao unaowagusa maisha yao hiyo pia ni uharakati.

SOF: Okay

AM: Ndio.

SOF: Na ufeminia kwa upande wangu mimi kwa sababu kwanza huwezi kujitambua kama wewe mwanamke na huwezi kujiamini katika kazi zako kwa sababu kwa mwanzo mimi sikuwa boss kazini, mimi nilikuwa mtu wa tatu katika kazi. Nilikuwa na boss wangu mwanaume alafu kuna boss mwanamke, huyu boss mwanaume alikuwa ananinyanyasa sana mfano kunitaka kimapenzi lakini kwa sababu mimi nilikuwa najitambua na sikuja kwa sababu yake na yeye sio aliyeniajiri na mimi nilikuwepo na kazi yangu na walinitoa kwenye kazi yangu na kunileta hapa. Kwa hiyo mimi nilikuwa najua thamani yangu kwa hiyo nikaweza kupigana kama mwanamke na nikasima kwa hivyo sasa mimi hivi nimekuwa boss. Kwa hiyo kuwa mwanamke na kuwa mwanaume boss juu si sababu za kuweza kuzalilika wewe mwanamke unatakiwa ujitambue wewe ni nani na ujue thamani yako.

AM: Kabsa hapo umegonga point asante. Kwenye hii sehemu yetu ya tano mwingiliano wako wa kazi yako pamoja na takwa ya wanawake nchini pajoma na kimataifa. Yaan, je katika shughuli zako za kila siku kuna watu unaofanya nao kazi hapa hapa Tanzania na wale unaofanya nao kazi nje za nchi. Najua kanga zako na bidhaa zako zingine zinaenda nje ya mipaka. Je nini mchanganuo wako tathmini na matarajio ya ukuaji wa Ufeminia katika nchi nini mahusiano yako na asasi zingine za wanawake nchini, na wanaharakati wengine unaonaje kazi yako kuhusiana na takwa la wanawake. Tunapoongelea takwa la wanawake ni ile kama women movement zile network.

SOF: Kwa upande wa takwa la wanawake nina mahusiano na taasisi za wanawake kama TWCC kwa upande wa Dar es Salaam na kwa Zanzibar center pia nina mahusiano na organization South Africa ambao hao mimi hawanijui ila nawasiliana nao kwa mitandao nikitaka kuagiza materials naagiza kupitia kwao. Na pia tunabadilishana mawazo nawatumia samples zangu ambazo nazitengeneza,(bad connection) nawambia ndio naweza saa zingine nawafanyia kama hii nitafutieni hapo South Africa. Sasa watakitafuta wakikosa wataniambia Sabrina unakitoa wapi hiki nawaambia nakitengeneza mwenyewe kwenye kiwanda changu. Kwa hiyo mambo kama hayo kwa movement kwa wanawake nashirikiana nao na tunafanya kazi vizuri. Kwa mfano kwa biashara kama zangu na hotels tunakutana

tunazungumza tunashauriana. Na kwa upande wa Ufemenia kwenye biashara zangu kama nilivyokwambia kwanza kwenye biashara zangu napenda sana kuwashirikisha wanawake wenzangu. Kwa sababu najua wanawake wengi especially kwa sisi wazanzibar utamaduni zetu na mila zetu ni Waislamu inakuwa vigumu wanawake kuwa kama mimi. Kwa hiyo mara nyingi napenda kuwa nao ili niwahamazishe kwa kuwapa historia yangu ya maisha vitu nilivyovipitia ili na wao wenzangu waweze kupata wigo kwanini yeye kafika hapa sisi tusifike. Hiyo ndio Feminia kwa upande wangu kwa wanawake wenzangu na kwa upande wa harakati kwenye biashara zangu nakutana sana na watu mbalimbali kama kwenye hotels na mara nyingi sana watu wanaonisapoti mimi ni wanawake wenzangu. Na sanasana sio wanawake wa kizanzibar mimi napambana na wanawake wa nje. Kwa sababu wanawake wa nje wanakuwa na wigo na hamu, wanasema kwanini wewe mwanamke umefika hapa. Kwa hiyo wanahamu ya kuzidi mkono ili nifike mbali zaidi.

AM: Asante. Je kwa hapo ulipofikia maono yako ya asasi yako ni kufikia wapi?

SOF: Kwa hapa nilipofikia, hapa ndio kwaanza naanza safari yangu kwa sababu hapa niko katika government zone nimekodi ni sehemu ya serikali ya viwanda. Mtazamo wangu niwe na sehemu yangu mwenyewe binafsi niweze kujenga na kuajiri watu wengi zaidi na kuweza kupanda miti kama migomba. Kuweza kuanza kutengeneza vitu ambavyo ni organic vinavyotokana na mimea na nikianza kufanya kitu kama hicho nitaweza kuajiri watu wengi na pia nitafika mbali zaidi. Na pia nataka niweze kufika mbali niuze vitu kimataifa sasa hivi nauza vitu vidogo lakini nataka niuze vingi zaidi pia target yangu sio kuuza quantity mimi nataka niuze kidogo ila iwe quality. Na pesa ile ambayo mimi nimeipanga kulingana na thamani ya kazi yangu, hiyo ndio target yangu kwa biashara yangu. Sitaki kuuza quantity kama vile watu wanaleta dump kutoka China hapana kwa sababu nalenga wateja wangu ambao hao wateja napambana nao kama hawa wanataka linen kwa hiyo ubora kwangu ndio kitu ambacho ni muhimu sana na ambacho nakipigania na nataka nifike mbali zaidi. Niondoke katika sehemu hii ya kupanga nataka niwe na sehemu yangu mwenyewe binafsi na niajiri wanawake wengi zaidi. Kwa sababu nahamazisha wanawake kwa sababu sasa hivi namhitaji mwanaume lakini nataka awepo mwanamke ambaye ataweza kusimama pale katikati asiwepo mwanaume. Kwa sababu mwanaume ukimpa oda na wewe mwanamke ni mdogo anakuwa hakuheshimu sasa akiwepo mwanamke kwa mwanamke inakuwa kiswahili chenu mnafahamiana na rahisi kufanya kazi.

AM: Asante sana nimefurahi uliposema una mtu ambaye anakusaidia kukata lakini target yako ni kumuweka mwanamke kwenye hizo kazi ambazo zimezoeleka kufanywa na wanaume.

SOF: Ndio.

AM: Asante, kwa kumalizia sasa umegusia muunganiko wako wa kimataifa katika harakati zako, je una mahusiano na wanaharakati wengine wa asasi mbalimbali katika nchi zingine zaidi ya Tanzania na kama zipo je zimekuwa na mchango gani katika kazi yako na je kuna utofauti gani na mahusiano kati ya vitu vinavyopigiwa kelele na mikakati inayochukuliwa na wanataalum au watu wa asasi mbalimbali.

Hapa ukilinganisha na nchi nyingine? Maana yake kule mwanzo umegusia una hayo mashirikiano na watu wa nje.

SOF: Ndio, nina mahusiano na watu wa nje kwa sababu hichi kiwanda wenyewe ni wa Swedish ambao walikuwa wamiliki sasa mmiliki ni mimi lakini bado wako na mimi kwa sababu wao unajua wenzetu western wakishaona kitu kimesimama wanahamu ya kuzidi kukusaidia zaidi kwa kusema oh! tumekianzisha hiki na bado kitu kimesimama na kuzidi kukua. Kwa hiyo nina vitu vingi mimi kwa sababu naagiza nje labels, zip, business card mimi business cards ziagizii Tanzania wala kenya zinatoka Sweden wao ndio wanonifanyiaoda kule na kuzituma kwangu. Na mabli na hao kuna watu wengine wako Holand pia wanakuwa wananiletea vitu siwajui hawa watu ni kama tu wewe ulivyonitafuta mimi na wao pia wamenitafuta mimi. Natuma pesa wananiletea mzigo ni wengi kuna wengine wako Denmark kuna wengine wako Marekani. Kwa hiyo nina watu tofauti ama watu wananitafuta tu tunaweza kutana tunashauriana nini cha kufanya ni vitu kama hivyo. Na pia utakuta wenzetu hawapendi mambo ya unyanyasaji wa kwetu sisi nchi zisizoendelea unyanyasaji kwa wanawake ni mkubwa sana. Lakini mimi nasema kikubwa zaidi ni sisi kuweza kujitambua na kujithamini. Tukiweza kujitambua na kujithamini kama sisi wanawake hakuna ambaye ataweza kutunyanyasa tusitegemee free lunch kuna wanawake tunaopenda sana kupewa vitu bure tusitegemee vya bure tuweze kujitoa tuweze kujituma tuweke mikakati yetu ya mipango ya muda mrefu. Na kwa uwezo wa Mungu tutafika hakuna lisilowezekana kwa Mungu tusipende kutegemea watu tutafika tu kwa uwezo wa Mungu.

AM: Asante, hello unanisikia?

SOF: Hello nakusikia

AM: Asante, labda kwa kumalizia tu nikuulize swali unaweza kutuelezea kidogo tu kwa ufupi kuhusu maisha yako, Ulisema ulikuzwa na mama ndio akakuhamazisha ukaingia kwenye NGOs baada ya kumaliza A level. Labda utupe ile snapshot ya maisha yako.

SOF: Okay. Maisha yangu mimi ni mzanzibar na mama ni mzanzibar na amenikuza yeye peke yake aliponizaa babangu aliniacha mimi nikiwa na miaka minne. Na sisi tuko watoto watatu katika familia yetu na mama yetu alikuwa mfanya biashara kwa hiyo mimi biashara itakuwa nimerithi kutoka kwa wazazi wangu na sikujua kwamba nilikuwa na hicho kitu lakini hicho kitu wamekuja kunijua hawa waliokuja kuniajiri kikazi. Na mamangu ni mwanaharakati kama mimi alikuwa anafanya kazi na anafanya biashara na nimekua mimi tulikuwa bado hatuna nyumba mamangu akanunua kiwanjwa baada ya mimi kupata kazi tukashirikiana na mama yangu tukajenga nyumba yetu. Kwa sasa tunakaa kwenye nyumba yetu na mamangu sasa hivi haishi Zanzibar yuko Oman pamoja na ndugu yangu mwanaume. Nina watoto watatu mtoto wangu wa kwanza ana miaka 11, mtoto wangu wa pili ana miaka 8 na mtoto wangu wa tatu ana miaka 4. Na watoto mimi nawasomesha kama mamangu alivyonisomesha simtegemei mume wangu. Ndio maana nasema sisi wanawake tunaweza, tujikomboe, tujiamini na tujithamini. Tusione kuwa ujana jike ni aibu mwanamke ni sawa na mtu mwingine yeyote na sisi tumeumbwa kama walivyoumbwa wao ni sisi

wenyewe tu kujithamini, kujitambua na kujipangia mikakati yetu ya maisha jinsi gani tunataka tuwe. Tuwe na mikakati ya muda mrefu ndipo tutafanikiwa tusifanye short tufanye long term alafu tuwe tunazipitia wapi tumekosea tuweze kujirekebisha.

AM: Asante sana Sabrina. Sawli langu linguine labda la uchokozi ulianza kufanya kazi ukiwa na umri gani maana ulisema ulipomaliza tu high school.

SOF: Nimeanza kufanya kazi ilikuwa 2004 sasa hivi ni mika 18.

AM: Kwa hiyo ulianza kwenye NGO ndio ukahamia kwenye hii kampuni ulioko sasa hivi?

SOF: Ndio nilianza kwenye NGO na kwenye hiyo NGO tulikuwa hatuna NGO tulikuwa tunakutana Forodhani huku Zanziabr tunakutana Forodhani chini ya mti tunagawana kazi hapo Forodhani akatokezea mfadhili. Akatufadhili akatupa ofisi lakini tulianza kwenye mti kuanza kufanya harakati zetu. Na hapo kwenye mti tulikuwa tunasomeshana lugha ya kuweza kutembeza wageni sababu mimi nimesomea pia kutembeza wageni. Kuwaeleza historia ya Zanzibar wapi ilipoanza na si hapo tu hapo hapo pia nilikuwa nafanya kazi hotel hapo hapo nilikuwa nafanya kazi katika nyanja mbalimbali na ndio maana nikahamasika zaidi mpaka leo hapa nilipofikia.

AM: Kwa hiyo ulijifunza kuwa tour guide si ndio?

SOF: Ndio

AM: Ukajifunza lugha na ulijifunza lugha gani?

SOF: Mimi lugha kwa sababu tangu shule nilikuwa na lugha yangu ya kingereza nikajifunza kitaliano na kifaransa na kispanish hizo ndio lugha zilikuwa zinafundishwa hapo. Kwa hiyo kila mtu alikuwa anachukua lugha ambayo yeye mwenyewe anaipenda na kwake rahisi na ataweza kufanyia kazi. Sisi sote tuliosoma kila mtu ana maisha yake tuliokuwepo hapo kwenye mti wote kila mtu ana maisha yake.

AM: Kila mtu ana maisha yake unamaanisha kutoka kuwa tour guide mkawa na ofsi zenu wenyewe .

SOF: Ndio tukawa tuna ofisi wengine wanayo hotels

AM: Aah! Hongereni. Asante sana Sabrina nilitaka kujua kule mwanzo nilijua kama nilikosa kitu na nimepata sasa maana mara nyingi tour guide kule Zanzibar naona ni wanaume.

SOF: Ndio hamna wanawake mimi nilianza mapema lakini sasa kutokana na mchanganuo nilikuwa na mambo mengi ya kukimbilia. Kwa hiyo sikuweza tena kurudi kuwa guide nikaendelea na safari nyingine.

AM: Okay! Asante sana. Haya dada Sabrina asante sana kwa muda wako.

SOF: Asante na wewe, shukuran sana.

AM: Asante na karibu.

SOF: Haya karibu sana.